


# Ubia wa Mnyororo wa Thamani kwenye Maziwa

## Muhtasari

Tanzania ina rasilimali za kutosha za ng'ombe wa maziwa ambazo zinaweza kubadilisha hali ya maisha na vipato kwa wakulima wadogo ndani ya mnyororo wa thamani. Hata hivyo, uzalishaji wa maziwa ya ng'ombe wa hapa nchini ni mdogo (lita 1-3/ng'ombe) na tasnia ya maziwa ni ndogo sana.. Kiasi kikubwa cha maziwa hutumika katika kaya zetu bila kufikia soko la biashara: ni kiasi cha asilimia 2 – 5 ya maziwa huzalishwa na wafugaji wakubwa au kwenye mashamba makubwa ya mifugo.

Sekta ya maziwa nchini Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuimarisha usalama wa chakula na lishe nchini. Mahitaji ya soko la maziwa yamekuwa kwa kipndi cha miaka kumi iliyopita na inakadiriwa kuwa mahitataji haya yataongezeka kulingana na mabadiliko chanya ya kijamii na kiuchumi.

Ili kushughulikia changamoto na fursa katika sekta ya maziwa, Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa kusini mwa Tanzania na wabia wake wameanzisha Ubia Mkakati wa Mnyororo wa Thamani kwenye Maziwa. Mpango huu unatekelezwa kwenye kongani ya Ihemi, ambapo wakulima wadogo 4,000 wanazalisha maziwa ghafi na kuyauza kwenye kiwanda cha kusindika maziwa cha ASAS na wakulima wadogo 820 wanazalisha maziwa ghafi na kuyauza kwenye kiwanda cha kusindika maziwa cha Njombe Milk Factory.

Kampuni za ASAS Dairies Ltd na Njombe Milk factory kwa sasa zinachakata maziwa chini ya uwezo wao. Kupitia Ubia uliopo katika Mnyororo wa Thamani wa Maziwa ushiriki wa wakulima wadogo umeimarika kiasi cha kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maziwa yenye ubora wa hali juu ambayo yatawezesha kukidhi uwezo kamili viwanda hivyo wa usindikaji wa maziwa..

## Nini kinasababisha ubia wa maziwa kuwa ubia mkakati ?

- **Kuimarika kwa usalama wa chakula na hali ya maisha katika kaya**
Ubia wa Mnyororo wa Thamani kwenye Maziwa utawaingiza wakulima wadogo kwenye mnyororo wa thamani na kubeba jukumu kubwa la kuboresha hali ya usalama wa chakula na lishe kwa kuongeza upatikanaji wa bidhaa zitokanazo na maziwa zenye virutubisho vya lishe.

- **Kutafuta masuluhisho ya kudumu katika mnyororo wa thamani**
Ubia wa Maziwa ulianzishwa kimkakati ili kujumisha wadau kutoka kila eneo linalohusisha mnyororo huu kubaini fursa za kuongeza thamani na kuukuza tija katika uzalishaji wa maziwa

- **Kuwakutanisha wabia** Ubia wa Maziwa unajumuisha wadau mbalimbali kama wasindikaji, wauzaji, wakulima wadogo na Serikali

- **Athari pana.** Ubia unatarajia kuwasaidia wakulima wapatao 4,820 na pia kuwafikia wengi zaidi katika kongani nyingine za SAGCOT

- **Kuonyesha athari chanya za kimazingira.** Wabia watashirikiana na wakulima kuhakikisha utunzaji wa rasilimaji ikiwemo pia kutumia mbinu za kilimo zinazohifadhi na kuboresha rutuba ya udongo

## Mpango wa Kukuza Kilimo kwenye Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT)

Mpango waSAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaolenga kuchochea Uwekezaji kwenye Kilimo biashara katika ukanda wa kusini mwa Tanzania. Kituo cha SAGCOT kinafanya kazi kama dalali wa ubia na kitovu cha habari kwa wabia wa SAGCOT katika kuwezesha uwekezeshaji kwenye minyororo ya thamani inayoshirikisha jamii na kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira. Kila mwaka, aina mabalimbali za ubia mkakati zimeibuka ambazo Mpango wa SAGCOT unashiriki kikamilifu kukuza na kuwezesha kutokana na Matukio makuu na yanayoweza kupanua shughuli hizi



## Wadau muhimu walioko kwenye Ubia wa Maziwa

- ASAS Dairies
- Njombe Milk factory
- Heifer-Tanzania
- ILRI
- ICRAF
- CIAT
- Technoserve
- AgriProfocus-Tanzania
- BODI YA MAZIWA TANZANIA
- WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
- Serikali za Mikoa Kongani na Ihemi
- Tanzania Milk Processors Association (TAMPA)
- Tanzania Milk Producers Association (TAMPRODA)
- GAIN
- Mamlaka ya Vyakula na Madawa Tanzania
- Shirika la Viwango Tanzania
- Taasisi za utafiti na mafunzo ya Maziwa



## Matukio Shirikishi na Endelevu

Kampuni za ASAS Dairies na Njombe Milk factory tayari zinafanya kazi na wakulima wadogo katika ukanda ya Nyanda za Juu Kusini kukusanya na kusindika maziwa.. Makampuni haya mawili hukusanya maziwa kutoka kwa wakulima wadogo katika mkoa ya Iringa, Njombe na Mbeya (Wilaya ya Ryngwe) takribani umbali wa kilomita 400 kutoka kiwanda cha usindikaji Iringa mjini.. Idadi ya walulima wadogo 4,820 wanashirikian na makampuni haya mawili.

Pamoja na hilo, ili kuhakisha kuwa mradi unaendeshwa kwa kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira, ubia huu utahusisha programu ya usimamizi wa maliasili, ikiwemo matumizi ya gesi taka, njia za kurutubisha udongo kwa kutumia samadi ya ng'ombe na kuhifadhi udongo kwa kutumia nyasi za kulishia mifugo ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.



## Changamoto na Hatua Zitakazochukuliwa

Kwa wakati huu tasnia ya mziwa nchini Tanzania ipo katika hatua ya awali, huku uzalishaji mkubwa wa maziwa ukiwa kwenye ngazi ya kaya. Utaalamu mdogo wa teknolojia ya maziwa, matumizi madogo ya programu za uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa kuboresha vinasaba na kuongeza uzalishaji pia yameathiri mnyororo wa thamani wa maziwa. Pamoja na hayo, wakulima wadogo wanaofuga ng'ombe wa maziwa wametawanyika katika maeneo mapana, ni vigumu kuwafikia na kukusanya maziwa ghafi kwa njia yenye ufanisi. Hivyo basi, Ubia kwenye Mnyororo wa Thamani wa Maziwa unafanya kazi kwa karibu zaidi na wakulima wadogo kuwasaidia waingie kwenye mchakato wa uzalishaji .

Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) unajikita kuitisha mkutano wa kikundi kazi katika Kongani ya Ihemi ili kusaidiana na wadau wa maziwa katika ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya maziwa. Kikundi kazi hiki kinaratibu kazi/shuguli miongoni mwa wanachama kupitia mkutano kuanzisha mpango kazi.

Ubia kwenye Mnyororo wa Thamani wa Maziwa pia unapanga kushirikisha wabia wa kifedha katika mpango huu ili kusaidia maendeleo ya vyombo vya kifedha vinavyofaa kwa ajili programu za wakulima wadogo zinazoimarisha teknolojia pamoja na vifaa/ vitendea kazi.

## Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:


SAGCOT Centre Limited

Gholofa ya 5, Jengo la Ikon
Bains Avenue, Masaki
S.L.P 80945
Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 260 1024
+255 22 260 0146
**Faxi:** +255 22 260 2368

**Barua Pepe:** info@sagcot.co.tz
**Tovuti:** www.sagcot.co.tz